

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO



KOTESHENI NAMBA.

LGA.161/2022/2023/W/132 LOT 04

Kwa ajili ya:

KAZI YA UJENZI WA MADARASA SABA (7) KATIKA SHULE YA MSINGI MATANDALANI

Tarehe: 20/04/2023

Kwa: LOCAL FUNDI WOTE NA WANANCHI WOTE:

1. Kotesheni (MK) unafuata Tangazo la ujenzi wa vyumba saba (7) vya madarasa kwa mwaka wa fedha **2022/2023**.
2. Shule ya msingi Matandalani imepokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba saba (7) vya madarasa kwa mwaka wa fedha **2022/2023**. Inakusudiwa kuwa sehemu ya Mapato ya fedha hizo yataatumika kugharamia malipo halali ya kazi ya **ujenzi wa vyumba saba (7) vya madarasa katika shule ya msingi Matandalani**.
3. Kama itakavyo kubaliwa katika utekelezaji wa ujenzi huo chini ya muongozo wa Mhandisi wa Ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, malipo yatafanywa kulingana na maelewano ila yatazingatia gharama halisi za soko katika Mkoa wa Katavi.
4. Maelekezo ya kujaza Kotesheni ya kazi hii ya umaliziaji yanapatikana katika Ofisi ya Mwalimu Mkuu shule ya msingi Matandalani.
5. Mwombaji atafika Ofisi ya Mwalimu Mkuu ili kuchukua kotesheni iliyo na orodha ya mahitaji na bei (BoQ) na ramani iliyo wazi kwa ajili ya kwenda kujaza bei ya kila kipengele.
6. Maombi yote yawe na nakala halisi (Original) moja iliyojazwa vizuri na kwa usahihi

Maombi yote yatumwe kwenda kwa Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Matandalani S.L.P 688, MPANDA.

bila kufuta kwa kutumia **kalamu ya bluu tu** na kusainiwa na mwombaji kila kurasa kisha kuwekwa kwenye bahasha nadhifu na iandikwe maandishi juu:

- 7. Maombi yatumwe kwenda kwa Mwalimu Mkuu Shule ya msingi Matandalani, S.L.P 688, Mpanda.**

8. MASHARTI YA MWOMBAJI NI KAMA IFUATAVYO; -

A. FUNDI WA KAWAIDA:

- a. Barua ya utambulisho kutoka serikali ya mtaa/kata/kijiji au kitongoji ambako mwombaji anatoka.
- a. Nakala ya kitambulisho cha kitaifa (NIDA) au cha mpiga kura.
- b. Nakala ya Tin – number kutoka TRA
- c. Mwombaji awe tayari kufanya kazi kwa muda utakaopangwa na kamati ya ujenzi kwa muongozo wa Mhandisi wa ujenzi.
- d. Barua ya maombi ya kazi.
- e. Nyaraka zinazoonesha uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi katika Taasisi za Umma au Taasisi Binafsi zinazotambulika.
- f. Vyeti vya ufundi kutoka (VETA) au taasisi nyingine za elimu ya ufundi zinazotambulika kisheria vitamuongezea mwombaji sifa Zaidi.
- g. Barua za maombi ya kazi, barua za wadhamini na nyaraka nyingine zote zichapwe na ziwasilishwe zikiwa katika mpangilio mzuri.
- h. Nyaraka za uzoefu wa kazi za ujenzi zinazofanana na kazi hii.
- i. Barua mbili za wadhamini zinazotambulika na serikali ya aidha mtaa/kata/kijiji au kitongoji ambako wadhamini hao wanaishi.
- j. Vyeti vya ufundi ujenzi kutoka kwenye taasisi zinazotambulika na serikali ya jamhuri ya muungano wa Tanzania vitamuongezea sifa muombaji.

B. TAASISI ZA UMMA:

- a. Wasifu wa wasimamizi watakao simamia mradi.
- b. Nyaraka za uzoefu wa kazi za ujenzi zinazofanana na kazi hii.
- c. Nakala ya Tin-number kutoka TRA.

9. Mwisho wa kuwasilisha Maombi ni Alhamisi ya tarehe **27/04/2023** kabla ya **saa nne kamili asubuhi**. Maombi yote yatafunguliwa hadharani kuanzia saa 4:00 Asubuhi katika ofisi ya Mwalimu Mkuu shule ya msingi Matandalani, **waombaji wote mnakaribishwa kuhudhuria kikoa cha ufunguzi**.
10. Angalizo maombi yote yatakayo chelewa, sehemu ya maombi, maombi ya kielektroniki, na maombi yasiyo funguliwa katika tukio la ufunguzi wa maombi, kwa hali yoyote ile hayatakubaliwa kwa tathmini.

.....

Elius D. Nguaro

MWALIMU MKUU